TANGAZO LA SERIKALI NA. 149 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA BONDENI SOKONI YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Bondeni Sokoni ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS1 yenye majira - nukta 535861MS, 8822389KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $72^{0}$ 11'08'' kwa umbali wa kilomita 1.492 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS2 yenye majira - nukta 537282MS, 8822846KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS3 yenye majira - nukta 537653MS, 8822548KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $51^{0}$ 12'46'' kwa umbali wa kilomita 0.475 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS4 yenye majira - nukta 538002MS, 8823078KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $33^{0}$ 21'02'' kwa umbali wa kilomita 0.63 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS5 yenye majira - nukta 536764MS, 8823844KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $58^{0}$ 16'31''kwa umbali wa kilomita 1.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BS6 yenye majira - nukta 535678MS, 8823672KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $08^{0}$ 08'15'' kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*